

MKUU WA WILAYA YA NYASA AWA MGENI RASMI KWENYE MAADHIMISHO YA MEI MOSI NYASA

Shirikisho la vyama vya wafanyakazi (TUCTA) Wilaya ya Nyasa vimempongeza Uongozi wa wilaya ya Nyasa mkoani Ruvuma kwa kuwa shirikishi ,unaojali maslahi ya wafanyakazi na kuhamasisha maendeleo wilayani hapa.

Hayo yameelezwa katika risala ya shirikisho la vyama vya wafanyakazi (TUCTA) wilaya ya Nyasa iliyosomwa katika maadhimisho ya siku ya wafanyakazi kiwilaya yaliyo fanyika katika viwanja vya Polisi Mbamba-bay jana Wilayani hapa.

Tucta wameafafanua kuwa Uongozi wa wilaya umekuwa ukihamasisha maendeleo na kukemea vitendo vya ukiukwaji wa sheria,na kanuni za utumishi wa Umma na kuhimiza idara zote hasa waajiri kuwajali wafanyakazi wa Wilaya ya Nyasa.

Aidha shirikisho hilo limeipongeza Serikali ya awamu ya tano kwa kutowavumilia wafanyakazi wasiofuata sheria taratibu na kanuni kwa kuwachukulia hatua za kinidhamu.

Akizungumza baada ya kupokea risala hiyo Mh.Isabela Chilumba alisema kuwa kila Mtumishi awajibike ipasavyo katika sehemu yake ya kazi na kwa uadilifu ili kuweza kutimiza malengo ya Serikali ya Awamu ya Tano

Aidha alisema ataendelea kutoa ushirikiano wa kutosha kwa wafanyakazi wote na kuwakaribisha katika ofisi yake pindi wanapokuwa na matatizo.